



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
SHIRIKA LA RELI TANZANIA**



Simu: 2133990
Telegram: Railways
Nukushi: 2133428

Ofisi ya Uhusiano
S.L.P 76959
Barabara ya Sokoine
Dar es Salaam

**TAARIFA KWA UMMA
KUWASILI KICHWA CHA TRENI YA UMEME**

Dar es Salaam, Tarehe 02 Novemba 2023

Shirika la Reli Tanzania – TRC linataarifu umma kuwa kichwa kipya cha treni ya umeme chenye namba ya usajili E6800-01 kilichoundwa na kampuni ya ‘*Hyundai Rotem Company*’ (HRC) kimewasili nchini Tanzania kutoka nchini Korea Kusini.

TRC iliagiza vichwa vipya 17 vya umeme kutoka ‘*Hyundai Rotem Company*’ (HRC) ya nchini Korea Kusini vyenye namba ya usajili E6800-01 hadi E6800-17 kwa ajili ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR. Mfumo wa uendeshaji unaotumika katika kichwa ni nishati ya umeme wenye msongo wa kilovoti 25 na kitakuwa na nguvu ya kilowati 5,000 sawa na nguvu ya 6,800 kwa kipimo cha ‘*Horse Power*’. Kichwa kitakuwa na uwezo wa mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa (160km/h), kuvuta na kulisha umeme kwenye mabehewa yasiyozidi 14 ya abiria kwa wakati mmoja.

TRC inatarajia kufanya majaribio ya kichwa cha treni kitakachotumika katika reli ya kiwango cha kimataifa kati ya Dar es Salaam na Morogoro na baadaye Dar es Salaam hadi Dodoma, baada ya kukamilisha ukaguzi wa kichwa na mafunzo ya uendeshaji kwa madereva mapema mwezi Disemba 2023.

Mwezi Disemba 2023 TRC inatarajia kupokea vichwa vingine vitatu (3), mpango wa uletaji vitendea kazi utakuwa ukitekelezwa kwa awamu pindi uundwaji wa vitendea kazi unapokamilika. TRC imeshapokea mabehewa 35 kwa ajili ya uendeshaji wa huduma katika reli ya kiwango cha kimataifa.

Kufikia Septemba 2023 mradi wa SGR Dar es Salaam – Morogoro umefikia 98.6%, Morogoro – Makutupora umefikia 95.41%, Makutupora – Tabora umefikia 12.32%, Tabora – Isaka umefikia 5.02% na Mwanza – Isaka umefikia 41.95%, Mkandarasi kampuni ya CCECC yuko eneo la mradi kwa ajili ya maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi wa SGR awamu ya pili Tabora - Kigoma.

Jamila Mbarouk
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano